

**UCHUNGUZI WA MFUATANO WA VIAMBISHI NAFSI KATIKA VITENZI VYA  
KISWAHILI NA KIARABU KWA KUZINGATIA ISIMU PAMBA NUZI**

Halima Ali Hassan

[halimaali749@gmail.com](mailto:halimaali749@gmail.com)

School of Swahili and Foreign Languages

*Department of Swahili*

**Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA)**

**Abstract:**

*The article aims to examine the sequence of subject pronoun affixes in the Swahili and Arabic verbs focusing on distinctive features. In this investigation, the relationship between Swahili and Arabic is first summarized. Then, this sequence of subject pronoun affixes in Swahili verbs is outlined, along with the sequence of subject pronoun affixes in Arabic verbs. Finally, a comparison is made, analyzing the similarities and differences in the sequence of subject pronouns affixes in the Swahili and Arabic verbs. The data analysis was guided by the principles of phrase structure grammar, established by Chomsky (1957). The article's data was obtained using the text reading method. This method enabled the researcher to identify Swahili and Arabic verbs used in the analysis. The research findings show that Swahili and Arabic share similarities and differences in the sequence of subject pronouns affixes in verbs. Both Swahili and Arabic are agglutinative languages that allow affixes to be attached to verbs. Subject pronoun affixes are found in both Swahili and Arabic verbs. The placement of these affixes takes into account the agent and the patient, as well as the number in both Swahili and Arabic. Despite the similarities in the attachment of subject pronoun affixes in Swahili and Arabic verbs. There is a significant difference in the rules governing the placement of these affixes in Swahili and Arabic. The sequence of subject pronoun affixes in Arabic is closely linked to gender (male and female), singular, dual and plural forms, as well as the distinction between the agent and the patient. Additionally, the subject pronoun affixes in Arabic take into account the tense of the action; and these affixes are placed at the end of the verb. In Swahili, subject pronoun affixes focus on singular and plural forms and also consider the agent or the patient. Therefore, we can observe that in Arabic, there is a much more extensive sequence of subject pronoun affixes attachment compared to Swahili.*

**Ikisiri:** Makala hii inalenga kuchunguza mfuatano wa viambishi nafsi katika vitenzi vya Kiswahili na Kiarabu kwa kuzingatia sifa pambanuzi. Katika uchunguzi huu, kwanza imeelezwa kwa muhtasari uhusiano uliopo kati ya Kiswahili na Kiarabu. Kisha, imebainishwa mfuatano wa viambishi nafsi katika kitende cha Kiswahili pamoja na kubainishwa mfuatano wa viambishi nafsi katika kitende cha Kiarabu. Mwisho, umefanyika ulinganishi kwa kuangalia kufanana na kutafautiana kwa mfuatano wa viambishi nafsi katika vitenzi vya Kiswahili na Kiarabu. Uchambuzi wa data uliongozwa na kanuni ya Sarufi Muundo Virai iliyoasisiwa na Chomsky mwaka (1957). Data za makala zimepatikana kwa kutumia mbinu ya usomaji wa matini. Mtafiti alisoma vitabu vya sarufi ya Kiswahili na vitabu vya sarufi ya Kiarabu. Mbinu hii

*ilimwezesha mtafiti kupata vitenzi vya Kiswahili na vitenzi vya Kiarabu vilivyotumika katika uchambuzi. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa Kiswahili na Kiarabu zinafanana na kutafautiana katika mfuatano wa viambishi nafsi katika vitenzi. Kiswahili na Kiarabu ni lugha ambishi zinazokubali kubeba viambishi katika kitenzi. Kiambishi nafsi hupatikana katika vitenzi vya Kiswahili na Kiarabu. Upachikaji wa viambishi hivyo huzingatia hali ya mtenda na mtendwa pamoja na kuzingatia hali ya idadi katika Kiswahili na Kiarabu. Licha ya kufanana katika upachikaji wa viambishi nafsi katika vitenzi vya Kiswahili na Kiarabu. Lakini kuna tafauti kubwa katika kanuni za upachikaji wa viambishi hivyo. Mfuatano wa viambishi nafsi katika Kiarabu umeshikamana na jinsia ya kieme na kike, idadi ya umoja, uwili na wingi pamoja na kuzingatia hali ya mtenda na mtendwa. Aidha, viambishi nafsi katika Kiarabu, huzingatia hali ya wakati wa kitendo, pamoja na viambishi hivyo kukaa mwishoni mwa kitenzi. Katika Kiswahili, viambishi nafsi huzingatia hali ya idadi ya umoja na wingi pamoja na kuzingatia hali ya mtenda au mtendwa. Hivyo, tunaweza kuona kuwa katika Kiarabu kuna mfuatano mpana mno wa upachikaji wa viambishi nafsi ukilinganisha na Kiswahili.*

Received: April 2024 202x, Accepted June 2024, Published: December 2024

© SUMAIT University Journal 2024

**Keywords:** kiambishi nafsi, sifa pambanuzi, sarufi miundo virai, Kiarabu, Kiswahili, mtendwa.

## 1.0 Utangulizi

Lugha za Kiswahili na Kiarabu zina historia ndefu ya mahusiano baina yao kiasi cha kuibuka nadharia tete kuhusu asili ya Kiswahili kuhusishwa na Kiarabu. Hata hivyo, kuna ushahidi wa kutosha unaothibitisha kuwa Kiswahili siyo Kiarabu bali ni mionganoni mwa lugha za Kibantu (Massamba, 2017:15). Mchanganyiko wa jamiilugha hizi mbili umesababisha kuwapo kwa maneno mengi ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu. Kuwapo kwa maneno hayo, kumechochea kufanyika tafiti kadhaa kuhusu athari ya Kiarabu katika Kiswahili. Wapo watalamu wanaothibitisha kuwa Kiswahili ni lugha yenye asili ya Kibantu lakini kimeathiriwa mno na Kiarabu kutokana na utohozi wa misamiati yake (Krumm, 1940; Bosha, 1993; Lodhi, 2000; Hakimu, 2020). Kimsingi, hoja zote hizi zinazothibitisha athari ya Kiarabu katika Kiswahili zinaacha upenyo wa kuchunguza zaidi uhusiano uliopo kati ya Kiswahili na Kiarabu.

### 1.1 Dhana ya Mfuatano wa Viambishi nafsi katika Kitenci


Attia (2002) anasema kuwa mfuatano wa viambishi ni mahusiano baina ya maneno ambayo yanashirikiana katika maumbo ya kimofosintaksia. Mahusiano hayo hupatikana katika jinsia, idadi, nafsi na njeo katika neno. Tunaweza kusema kuwa mfuatano wa viambishi katika kitenzi ni ule ukubalifu wa vipashio vya kisarufi vinavyotumika kubainisha mahusiano ya kategoria zinazounda kitenzi. Kitenci huundwa kutokana na viambishi mbalimbali ambavyo huwekwa pamoja kwa kuzingatia sifa pambanuzi za lugha husika. Massamba (2016:115) anasema kuwa sifa pambanuzi ni sifa ambazo hutumika katika kukitofautisha kipashio cha kiisumu na vipashio vyengine vya aina yake. Kila kipashio kimoja huwa na sifa yake kwa kuzingatia muktadha wa umbo husika. Viambishi ni mofimu zinazoambatanishwa kwenye mzizi wa neno ili kuwakilisha hali au dhana mbali mbali zinazofungamana na neno pamoja na mofimu hizo (Kihore na wenzake, 2001:65). Viambishi nafsi ni kategoria ya kisarufi ambayo hubainisha nafsi ya mtenda/mtendi na mtendwa. Mtendi ni nomino inayohusika na kufanya tendo linaloelezwa katika kitenzi na mtendwa ni nomino inayoathirika moja kwa moja na tendo linaloelezwa katika kitenzi (Massamba, 2016:83).

## **2.0 Kiunzi cha Nadharia**

Kanuni ya Sarufi Miundo Virai iliasisiwa na Chomsky (1957) ili kurekebisha taratibu za sarufi za awali. Kanuni hii huchambua virai kwa kuangalia vijenzi vyake na kuviainisha. Lengo kuu la kanuni ya Sarufi Miundo Virai ni kufafanua makundi ya kisarufi kwa kuonesha uhusiano kati yake. Kanuni hii hujikita katika uandikaji upya wa sheria za sarufi ambazo hudhihirisha nafasi na uamilifu wa vijenzi vya sentensi, kuanzia kiambajengo kikubwa (sentensi) hadi kiambajengo kidogo (sauti). Mkabala huu pia hutumia dhana ya upanuzi. Dhana hii huhusu ule uwezekano wa kitengo fulani kuwakilishwa na kingine na kikaendelea kuhifadhi ukubalifu wa kisarufi (Massamba na wenzake, 2012:58). Naye, Attia (2002:47) anafafanua kanuni tatu zinazopatikana katika kanuni ya Sarufi Miundo Virai kwa kutumia mfano ufuatao {the young boy eats the apples} ‘mvulana mdogo anakula tufaa’ anaeleza kuwa:

‘There are three types of relationships that can be captured by syntactic description. The first is the relationship of ‘sequence’ which states which elements precede other elements. In the above tree, for example, the adjective young precedes the noun boy, which it modifies. The second type of relationship is ‘dependence’ which states that some elements are dependant on other elements. For example, the preposition can determine the morphological form (or case) of the noun that follows it, as in to him, in which case the pronoun is dependant on the preposition. In the above example, the noun boy and the verb eats both agree in number, an example of the verb dependence on the subject. The third type of relationship is ‘constituency’ which means that some elements may be combined together to constitute a phrase. In the above example, the first NP consists of Det, Adj and N. These are some of the basic concepts needed in syntactic analysis’.

Kuna aina tatu za mahusiano ambayo yanaweza kufafanuliwa katika maelezo ya kisintaksia. Aina ya kwanza ni uhusiano wa ‘mpangilio’ ambaao unaeleza ni vipengele gani vinavyotangulia vipengele vyengine. Kwa mfano, katika tawi liliopo juu, kivumishi ‘mdogo’ kimeitangulia nomino ‘mvulana’ ambayo inairejelea. Aina ya pili ya uhusiano ni ‘utegemezi’ ambaao unaeleza kuwa baadhi ya vipengele vinategemea vyengine. Kwa mfano, kihuishi kinaweza kuamua umbo la kisarufi (au kisa) cha nomino inayofuata, kama ilivyo, katika hali hii, kiwakilishi huwa kina utegemezi katika kihuishi. Katika mfano uliopo juu, nomino ‘mvulana’ na kitendo ‘anakula’ vyote vina ukubalifu wa idadi, kwa mfano kitendo huwa na utegemezi wa mtenda. Aina ya tatu ya uhusiano ni ‘muunganiko’ wenye maana ya kuwa baadhi ya vipengele huungana pamoja ili kuunda kirai. Katika mfano uliopo juu, kirai nomino cha kwanza kimeshikamana na kibainishi, kivumishi na nomino. Hizi ni baadhi ya dhana za msingi zinazohitajika katika uchambuzi wa kisintaksia (tafsiri yetu). Kutokana na kanuni ya upanuzi wa maneno ya Sarufi Miundo Virai tunaweza kuainisha kama ifuatavyo:



a-nafsi ya tatu, umoja, mtenda.

Kanuni hii ya Sarufi Miundo Virai inakwenda sambamba na lengo la makala la kuchunguza mfuatano wa viambishi nafsi katika vitenzi vya Kiswahili na Kiarabu. Nadharia hiyo, imetumika katika

uchambuzi wa mfuatano wa viambishi nafsi katika kitenzi cha Kiswahili na Kiarabu. Mtafiti ametumia njia ya jedwali, mishale na maelezo katika uchambuzi wa mfuatano wa viambishi nafsi katika kitenzi cha Kiswahili na Kiarabu.

### 3.0 Uchambuzi wa Data

Ili kuweza kufanya ulinganishi wa viambishi nafsi katika vitenzi vya Kiswahili na Kiarabu. Makala hii imegawanywa katika sehemu tatu ambazo ni ubainishaji wa kiambishi nafsi katika kitenzi cha Kiswahili, halafu Kiarabu na mwishoni ubainishi wa kufanana na kutafautiana kwa kiambishi nafsi katika Kiswahili na Kiarabu.

#### 3.1 Kiambishi Nafsi katika Kitenzi cha Kiswahili

Kiambishi nafsi katika nafasi ya kiima ni nafasi ya mtenda/mtendi (yaani ile inayotenda tendo) na kiambishi nafsi katika yambwa ni kiambishi nafsi ya mtendwa (Kihore na wenzake, 2001).

#### Jedwali Na.1 Kiambishi Nafsi katika Vitenzi vya Kiswahili-Mtenda

| Kiakilishi<br>Nafsi | Kitenzi  |          | Kiambishi Nafsi |       |
|---------------------|----------|----------|-----------------|-------|
|                     | Umoja    | Wingi    | Umoja           | Wingi |
| N <sub>1</sub>      | nimerudi | tumerudi | ni-             | tu-   |
| N <sub>2</sub>      | utakuja  | mtakuja  | u-              | m-    |
| N <sub>3</sub>      | analala  | wanalala | a-              | wa-   |

#### Nafsi ya Kwanza

Nafsi ya kwanza hii ni kategoria ambayo huonesha kuwa msemaji anajirejelea mwenyewe au kundi la watu ambalo msemaji yumo. Nafsi hii huwakilishwa na kiambishi patanishi {ni-} katika umoja na kiambishi patanishi {tu-} katika wingi.

#### Nafsi ya Pili

Nafsi ya pili ni kategoria ambayo hudhihirisha kuwa msemaji anamrejelea mtu au kundi la watu ambalo lipo karibu na alipo. Huwakilishwa na kiambishi patanishi {u-} katika umoja na katika wingi huwakilishwa na kiambishi patanishi {m-}.

#### Nafsi ya Tatu

Nafsi ya tatu ni kategoria ambayo hudhihirisha kuwa msemaji anamrejelea mtu ambaye hayupo au yupo mbali na alipo. Katika Kiswahili nafsi ya tatu huwakilishwa na kiambishi patanishi {a-} katika umoja na kiambishi patanishi {wa-} katika wingi.

Tunaweza kuainisha kwa kutumia kanuni ya Sarufi Miundo Virai kwa njia ya mishale kama ifuatavyo:

Ni me rud i

|      |      | -kiambishi tamati  
 |      |      | rud-mzizi  
 |      |      | me-wakati uliopita (muda mchache)  
 ni-N<sub>1</sub>.umoja, mtenda.

#### Jedwali Na. 2 Kiambishi Nafsi katika Kitenzi cha Kiswahili-Mtendwa

| Kiakilishi<br>Nafsi | Kitenzi   |             | Kiambishi Nafsi |                              |
|---------------------|-----------|-------------|-----------------|------------------------------|
|                     | Umoja     | Wingi       | Umoja           | Wingi                        |
| N <sub>1</sub>      | amenipiga | ametupiga   | -ni- awali)     | -tu- (awali)                 |
| N <sub>2</sub>      | amekupiga | amekupigeni | -ku-(awali)     | -ku- (awali)<br>-ni (tamati) |
| N <sub>3</sub>      | amempiga  | amewapiga   | -m- (awali)     | -wa- (awali)                 |

## **HALIMA ALI HASSAN: UCHUNGUZI WA MFUATANO WA VIAMBISHI NAFSI KATIKA VITENZI VYA KISWAHILI NA KIARABU KWA KUZINGATIA ISIMU PAMBA NUZI**

Kiambishi nafsi awali {-ni-} hupachikwa katika nafsi ya kwanza umoja na katika hali ya wingi hupachikwa kiambishi nafsi {-tu-} kubainisha mtendwa. Kiambishi nafsi awali {-ku-} hupachikwa kabla ya mzizi wa kitenzi katika nafsi ya pili ya umoja pamoja na kiambishi tamati {-ni-} ambacho hupachikwa mwishoni mwa mzizi. Katika nafsi ya tatu, hupachikwa kiambishi awali {-m-} katika hali ya umoja na katika hali ya wingi hupachikwa kiambishi awali {-wa-}.

Tunaweza kuainisha kwa kutumia kanuni ya Sarufi Miundo Virai kwa njia ya mishale kama ifuatavyo :

### **3.2 Mfuatano wa Viambishi Nafsi katika Kitenzi cha Kiarabu**

Katika lugha ya Kiarabu, kiambishi nafsi tamati hupatikana katika kitenzi cha wakati uliopita na uliopo kwa kuzingatia hali ya mtenda na mtendwa. Kiambishi hiki hujulikana kwa jina la /dˤam:i:r mu'tasˤil/ (ضَمِير مُتَصلٌ). Navyo huwa na uzingativu wa nafsi ya mtenda, mtendwa, wakati, jinsia na idadi (JapenSarage na Kasiyarno, 2015).

### **Jedwali Na.3 Kiambishi Nafsi katika Kiarabu Wakati uliopita-Mtenda (N<sub>1</sub>-N<sub>2</sub>)**

Tunapoangalia jedwali iliyopo juu, tunaona kuwa viambishi nafsi tamati vinapatikana baada ya mzizi wa kitenzi. Hivyo, tunaweza kusema kuwa hakuna kiambishi nafsi awali katika kitenzi cha wakati uliopita. Kiambishi nafsi tamati katika kitenzi kilichopita hupatikana katika miktadha ifuatayo:

- Kiambishi nafsi tamati ‘tau ya mtenda’ /tau l-fa:ڦil/, inapatikana katika kitenzi cha wakati uliopita katika nafsi ya kwanza ya umoja pamoja na vitenzi vyote katika nafsi ya pili {كَتَبْتُ، كَتَبْتَ، كَتَبْتُمْ، كَتَبْتُمْ}.
- Kiambishi nafsi tamati ‘naa ya watenda’ /na:l-fa:ڦili:na/, inapatikana katika wingi wa nafsi ya kwanza {كَتَبْنَا}.
- Kiambishi nafsi tamati ‘alif ya uwili’ /alifu l-θnain/ {أَلْفُ الْاثْنَيْنِ} inapatikana katika kitenzi kilichofanywa na nafsi ya pili katika hali ya uwili {كَتَبْنَمَا}.

#### Jedwali Na. 4 Kiambishi Nafsi Wakati Uliopita Mtenda (N<sub>3</sub>)

| Kiwakilishi Nafsi                 |     | Mifano ya kitenzi |            | Kiambishi Nafsi   |   | Tafsiri kwa Kiswahili  |
|-----------------------------------|-----|-------------------|------------|---|---|------------------------|
| N <sub>3.umaja.mm</sub><br>(yeye) | هو  | /kataba/          | كتَبَ      | Kiambishi nafsi fiche cha nafsi ya tatu, umoja wa kiume | هو-الضمير الغائب المفرد المذكر، مستتر             | aliandika (mm)         |
| N <sub>3.umaja.kk</sub><br>(yeye) | هي  | /katabat/         | كتَبْتُ    | Kiambishi nafsi fiche cha nafsi ya tatu, umoja wa kike  | هي-الضمير الغائب المفرد المؤنث، مستتر             | aliandika (kk)         |
| N <sub>3.uwili.mm</sub>           | هما | /kataba:/         | كتَبَنا    | alifu ya uwili katika nafsi ya tatu, uwili wa kiume     | أَلْفُ الْاثْنَيْنِ- الضمير الغائب المثنى، المذكر | waliandika (mm)        |
| N <sub>3.uwili.kk</sub>           | هما | /katabata:/       | كتَبْنَا   | alifu ya uwili katika nafsi ya tatu, uwili wa kike      | أَلْفُ الْاثْنَيْنِ-الضمير الغائب المثنى، المؤنث  | waliandika (kk)        |
| N <sub>3.wingi.mm</sub>           | هم  | /katabu:/         | كتَبُوا    | wau ya wingi katika nafsi ya tatu, wingi wa kiume       | وَالْجَمَاعَةِ-الغائب الجمع المذكر                | waliandika (wengi, mm) |
| N <sub>3.wingi.kk</sub>           | هنّ | /katabna/         | كتَبْنَاهُ | nuun ya kike katika nafsi ya tatu, wingi wa kike        | نَوْنَ النَّسْوَةِ-الغائب الجمع المؤنث            | waliandika (wengi, kk) |

Vitenzi nya wakati uliopita hufuatana na viambishi nafsi tamati isipokuwa katika nafsi ya tatu ya umoja wa kiume /kataba/ {كتَبَ} ‘aliandika’ na katika umoja wa kike /katabat/ {كتَبْتُ} ‘aliandika’. Kitendo kinachofanywa na nafsi ya tatu katika umoja wa kiume huwa ndio jengo la msingi la kitenzi katika Kiarabu. Aidha, Kitenzi katika nafsi ya tatu, umoja wa kike /katabat/ {كتَبْتُ} huishia na tau yenye sukuun /tau ta?ni:θi sa:kinah/ {تَاءُ ثَانِيَّةٍ سَاكِنَةٍ}. Tau yenye sukuun ni alama inayooonesha jinsia

## **HALIMA ALI HASSAN: UCHUNGUZI WA MFUATANO WA VIAMBISHI NAFSI KATIKA VITENZI VYA KISWAHILI NA KIARABU KWA KUZINGATIA ISIMU PAMBA NUZZI**

ya kike wala sio kiambishi nafsi. Pia, tau yenyen sukuun hupatikana katika kitenzi cha nafsi ya tatu, uwili wa kike {كتبَتْ} ‘waliandika’ kabla ya kiambishi nafsi cha alif ya uwili او {ألفَ الآثينِ} (Iqaab, 2019). Aidha, Kiambishi nafsi tamati cha waau ya wingi /waau l-jama: ؓKatِ الجماعة}, hupatikana katika nafsi ya tatu, wingi wa kiume {كتبُوا ‘waliandika’, alifu inayoonekana katika mfano, huwa haitamkwi imekaa ili kusaidia kiambishi nafsi. Pia, hupatikana kiambishi nafsi cha nuun ya kike /nuu:n l-niswat/ نون النسوة katika nafsi ya tatu ya wingi wa kike {كتبَنْ}. Tunaweza kuainisha kiambishi nafsi kwa kutumia kanuni ya Sarufi Miundo Virai kwa njia ya mishale kama ifuatavyo:

katabtu l-kita:ba ‘niliandika kitabu’

kita:ba-mtendwa, irabu fatha  
al- herufi ya maarifa  
tu- kiambishi nafsi ya kwanza (mtenda)

katab-kitenzi cha wakati uliopita, chenyé irabu ya sukuun pahala pa fatha Tunaweza kubainisha kiambishi nafsi katika mtenda kisintaksia kwa kutumia hati za Kiarabu.

كتاب الكتب

**الكتاب** مفعول به منصوب بالفتحة (الـ دالة على معرفة) تـ ناء المتكلم- ضمير رفع متصل، مبني في محل رفع الفاعل كـ تـ بـ فعل ماض مبني على السكون في محل نصب

## **Kiambishi Nafsi katika Wakati uliopita-Mtendwa**

Kiambishi nafsi cha mtendwa hutumika katika kubainisha mtu aliyefanyiwa kitendo. Katika Kiarabu, kiambishi nafsi tamati cha mtendwa hupatikana mwishoni mwa kitenzi (Hahn, 2011). Viambishi nafsi nya mtendwa hupatikana katika makundi yote matatu ya viwakilishi nafsi ( $N_1$ ,  $N_2$  na  $N_3$ ).

#### **Jedwali Na.5 Kiambishi Nafsi katika Kitenzi cha Wakati uliopita-Mtendwa (N<sub>1</sub> na N<sub>2</sub>)**

| Kiwakilishi Nafsi           | Kitenzi wakati uliopita         | Kiambishi Nafsi   | Tafsiri   |
|-----------------------------|---------------------------------|---|---|
| N <sub>1.umaja</sub>        | أَنَا /dˤarabənii/ ضَرَبَنِي    | /nii/ kiambishi nafsi ya kwanza katika umaja wa mtendwa       | -ني-<br>الضمير المتكلم المفرد - دالة على المفعول به<br>alnipiga               |
| N <sub>1.wingi</sub>        | أَنْحُنْ /dˤarabana:/ ضَرَبَنَا | /naa/ kiambishi nafsi ya kwanza katika wingi wa mtendwa       | نا- الضمير المتكلم الجمع،<br>دالة على المفعول به<br>alitupiga                 |
| N <sub>2.umaja.</sub><br>mm | أَنْتَ /dˤarabaka/ ضَرَبَكَ     | /ka/ kiambishi nafsi ya pili katika umaja wa kiume wa mtendwa | كـ- الضمير المخاطب المفرد<br>المذكر، دالة على المفعول به<br>alikupiga<br>(mm) |

|                             |           |                             |            |   |   |                         |
|-----------------------------|-----------|-----------------------------|------------|---|---|-------------------------|
| N <sub>2.umaja.</sub><br>kk | أُنتَ     | /d <sup>f</sup> arabaki/    | ضرَبَكِ    | /ki/ kiambishi nafsi ya pili katika umaja wa kike wa mtendwa    | كِ- الضمير المخاطب المفرد المؤنث- دالة على المفعول به   | alikupiga (kk)          |
| N <sub>2.uwili</sub>        | أَنْتُمَا | /d <sup>f</sup> arabakuma:/ | ضرَبَكُمَا | /kuma:/ kiambishi nafsi ya pili katika uwili wa mtendwa         | كُمَا- الضمير المخاطب المثنى، دالة على المفعول به       | alikupigeni (wawili)    |
| N <sub>2.wingi.</sub><br>mm | أَنْتُمْ  | /d <sup>f</sup> arabakum/   | ضرَبَكُمْ  | /kum/ kiambishi nafsi ya pili katika wingi wa kiume wa mtendwa  | كُمْ- الضمير المخاطب الجمع المذكر، دالة على المفعول به  | alikupigeni (wengi, mm) |
| N <sub>2.wingi.</sub><br>kk | أَنْتُنَّ | /d <sup>f</sup> arabakunna/ | ضرَبَكُنَّ | /kunna/ kiambishi nafsi ya pili katika wingi wa kike wa mtendwa | كُنَّ- الضمير المخاطب الجمع المؤنث، دالة على المفعول به | alikupigeni (wengi, kk) |

Tunapoangalia mifano iliyopo katika jedwali, tunaona kuwa viambishi nafsi vyta mtendwa katika Kiarabu vinajitokeza kama ifuatavyo :

- Kiambishi nafsi tamati /-ii/ ya mtendwa inayoungana na nuun {ني}, inapatikana katika kitenzi cha wakati uliopita katika nafsi ya kwanza umaja /d<sup>f</sup>arabanii/ {ضرَبَتِي} ‘alinipiga’. Kiambishi nafsi tamati /-na:/ kinapatikana katika nafsi ya kwanza katika wingi wa mtendwa /d<sup>f</sup>arabana:/ {ضرَبَنا} ‘alitupiga’.
- Kiambishi nafsi tamati /-ka/ kinapatikana katika nafsi ya pili katika umaja wa kiume /d<sup>f</sup>arabaka/ {ضرَبَكِ} ‘alikupiga’ na kiambishi nafsi tamati /-ki/ kinapachikwa katika nafsi ya pili ya umaja wa kike /d<sup>f</sup>arabaki/ {ضرَبَكِ} ‘alikupiga’.
- Kiambishi nafsi tamati /-kuma:/ kinachopachikwa katika nafsi ya pili ya uwili wa kike au wa kiume /d<sup>f</sup>arabakuma:/ {ضرَبَكُمَا} ‘alikupigeni’. Kiambishi nafsi tamati /-kum/ hupachikwa katika nafsi ya pili ya wingi wa kiume /d<sup>f</sup>arabakum/ {ضرَبَكُمْ} ‘alikupigeni’ na kiambishi /-kunna/ hupachikwa katika kitenzi kilichofanywa na nafsi ya pili ya wingi wa kike /d<sup>f</sup>arabakunna/ {ضرَبَكُنَّ} ‘alikupigeni’.

#### Jedwali Na.6 Kiambishi Nafsi cha Wakati uliopita-Mtendwa (N<sub>3</sub>)

| Kiwakilishi Nafsi           |    | Wakati uliopita          |         | Kiambishi Nafsi                           |                                  | Tafsiri       |
|-----------------------------|----|--------------------------|---------|---|----------------------------------|---------------|
| N <sub>3.umaja.</sub><br>mm | هو | /d <sup>f</sup> arabahu/ | ضرَبَهُ | /hu/ kiambishi nafsi ya tatu katika umaja | -هُ الضمير الغائب المفرد المذكر، | alimpiga (mm) |

**HALIMA ALI HASSAN: UCHUNGUZI WA MFUATANO WA VIAMBISHI NAFSI KATIKA VITENZI VYA KISWAHILI NA Kiarabu Kwa Kuzingatia Isimu Pambanuzi**

---

|                              |     |                             |            | wa kiume wa mtendwa  | دالة على المفعول به  |                          |
|------------------------------|-----|-----------------------------|------------|--|--|--------------------------|
| N <sub>3.umaja.</sub><br>kk  | هي  | /d <sup>r</sup> arabaha/    | ضرَبَهَا   | /ha/<br>kiambishi<br>nafsi ya tatu<br>katika umoja<br>wa kike wa<br>mtendwa    | ها-<br>الضمير الغائب<br>المفرد المؤنث،<br>دالة على<br>المفعول به | alimpiga<br>(kk)         |
| N <sub>3.uwili</sub>         | هما | /d <sup>r</sup> arabahuma:/ | ضرَبَهُمَا | /huma:/<br>kiambishi<br>nafsi ya tatu<br>katika uwili<br>wa mtendwa            | هما- الضمير<br>الغائب المثنى،<br>دالة على<br>المفعول به          | aliwapiga<br>(wawili)    |
| N <sub>3.wing.<br/>mm</sub>  | هم  | /d <sup>r</sup> arabahum/   | ضرَبَهُمْ  | /hum/<br>kiambishi<br>nafsi ya tatu<br>katika wingi<br>wa kiume wa<br>mtendwa  | هم- الضمير<br>الغائب الجمع<br>المذكر، دالة<br>على المفعول<br>به  | aliwapiga<br>(wengi, mm) |
| N <sub>3.wingi.<br/>kk</sub> | هنّ | /d <sup>r</sup> arabahunna/ | ضرَبَهُنّ  | /hunna/<br>kiambishi<br>nafsi ya tatu<br>katika wingi<br>wa kike wa<br>mtendwa | هنّ-<br>الضمير الغائب<br>الجمع المؤنث،<br>دالة على<br>المفعول به | aliwapiga<br>(wengi, kk) |

Kiambishi nafsi tamati /hu/ {هـ} hupachikwa mwishoni mwa kitenzi cha wakati uliopita ili kubainisha nafsi ya mtendwa. Kiambishi nafsi hiki hupachikwa katika jengo la msingi la kitenzi kilichofanywa na nafsi ya tatu, umoja wa kiume /d<sup>r</sup>arabahu/ {ضرَبَهُ} ‘alimpiga’. Kiambishi nafsi tamati /ha:/ {ها} hupachikwa mwishoni mwa kitenzi cha wakati uliopita ili kubainisha nafsi ya mtendwa katika hali ya umoja wa kike /d<sup>r</sup>arabaha/ {ضرَبَهَا}. Aidha, kiambishi nafsi tamati /huma:/ hupachikwa mwishoni mwa kitenzi cha wakati uliopita ili kubainisha nafsi ya watendwa wawili (wa kike au wa kiume) /d<sup>r</sup>arabahuma:/ {ضرَبَهُمَا} ‘aliwapiga’. Kiambishi nafsi tamati /hum/ {هم} hupachikwa mwishoni mwa kitenzi cha wakati uliopita ili kubainisha nafsi ya watendwa wengi wa kiume /d<sup>r</sup>arabahum/ {ضرَبَهُمْ} ‘aliwapiga’. Kiambishi nafsi tamati /hunna/ {هنّ} hupachikwa mwishoni mwa kitenzi cha wakati uliopita ili kubainisha nafsi ya watendwa wengi wa kike /d<sup>r</sup>arabahunna/ {ضرَبَهُنّ} ‘aliwapiga’.


Tunaweza kuainisha kwa kutumia kanuni ya Sarufi Miundo Virai.

/d<sup>r</sup>araba nii/ ‘amenipiga’

nii-kiambishi nafsi, mtendwa

d<sup>r</sup>araba-kitenzi cha wakati uliopita chenye fatha (mtenda).

Tunaweza kuainisha kiambishi nafsi kwa kutumia kanuni ya Sarufi Miundo Virai kwa kutumia hati ya Kiarabu kama ifuatavyo :



### **3.4 Kiambishi Nafsi katika Wakati uliopo-Mtenda**

Kitendo cha wakati uliopo katika Kiarabu hutambulika kwa jina la /fi<sup>ʕ</sup>ilu mud<sup>ʕ</sup>a:ri<sup>ʕ</sup>/ . Firmansyah (2022) anasema kuwa kitendo cha wakati uliopo ni kila tamko linalojulisha juu ya kufanyika kwa kitendo katika wakati uliopo au wakati ujao. Mtenda ni mtu ambaye amefanya kitendo katika lugha ya Kiarabu huitwa /fa:<sup>ʕ</sup>ilu/ {فَاعل}. Kitendo cha wakati uliopo ni lazima kianzie na herufi maalumu zinazobainisha hali ya wakati uliopo. Herufi hizo ni /alif/ {ا}, /nuun/ {ن}, /yau/ {ي} na /tau/ {ت} ambazo huitwa /huru:uf mud<sup>ʕ</sup>a:ri<sup>ʕ</sup>/ {حروف المضارعة}. Izingatiwe kuwa herufi hizo siyo viambishi nafsi bali ni viambishi vinavyobainisha hali ya wakati uliopo. Herufi hizi hupatikana katika viwakilishi nafsi vifuatavyo :

- a. Kiambishi awali /alif/ hupachikwa katika nafsi ya kwanza katika umoja {أنا} ‘mimi’

b. Kiambishi awali /nuun/ hupachikwa nafsi ya kwanza katika wingi {نحن} ‘sisi’

c. Kiambishi awali /ta/ hupachikwa katika nafsi zote za pili pamoja na nafsi ya tatu katika hali ya umoja wa kike na uwili wa kike /?anta/, /?anti/, /?antuma:/, /?antum/ {أنتما}, /?antunna/ {أنتنّ}, pamoja na /hiya/ {هي} na /huma:/ {همًا}.

d. Kiambishi awali /ya/ hupachikwa katika nafsi ya tatu {هم} na {هنّ} (isipokuwa katika nafsi ya tatu; uwili wa kike {هم} huwakilishwa na kiambishi /ta/).

#### **Jedwali Na.7 Kiambishi Nafsi cha Wakati uliopo, Mtenda (N<sub>1</sub> na N<sub>2</sub>)**

| Kiwakilishi Nafsi       | Kitendo cha wakati uliopo | Kiambishi Nafsi  | Tafsiri ya Kiswahili                                     |
|-------------------------|---------------------------|--|--|
| N <sub>1.umaja</sub>    | أنا /Paktubu/             | أكتبُ kiambishi nafsi fiche cha nafsi ya kwanza katika umaja (mimi)        | الضمير المتكلم المفرد، مستتر (أنا) ninaandika            |
| N <sub>1.wingi</sub>    | نحن /naktubu/             | نكتبُ kiambishi nafsi fiche cha nafsi ya kwanza katika wingi (sisi)        | -الضمير المتكلم- الجمع، مستتر (نحن) tunaandika           |
| N <sub>2.umaja.mm</sub> | أنتَ /taktubu/            | تكتبُ kiambishi nafsi fiche cha nafsi ya pili katika umaja wa kiume (wewe) | الضمير المخاطب المفرد المذكر مستتر (أنتَ) unaandika (mm) |

**HALIMA ALI HASSAN: UCHUNGUZI WA MFUATANO WA VIAMBISHI NAFSI KATIKA VITENZI VYA KISWAHILI NA Kiarabu Kwa Kuzingatia Isimu Pambanuzi**

|                         |        |              |             |  |   |                          |
|-------------------------|--------|--------------|-------------|--|---|--------------------------|
| N <sub>2.umaja.kk</sub> | أنتَ   | /taktubi:na/ | تُكْثِنَّ   | 'yau'<br>kiambishi nafsi<br>ya pili katika<br>umoja wa kike                  | ياء-الضمير<br>المخاطب المفرد<br>المؤنث            | unaandika<br>(kk)        |
| N <sub>2.uwili</sub>    | أنتما  | /taktuba:ni/ | تُكْثِبَانَ | 'alif ya uwili'<br>kiambishi nafsi<br>ya pili katika<br>hali ya uwili        | ألف الاثنين-<br>الضمير<br>المخاطب المثنى          | mnaandika<br>(wawili)    |
| N <sub>2.wingi.mm</sub> | أنتم   | /taktabu:na/ | تُكْثِبُونَ | 'waau ya<br>wingi'<br>kiambishi nafsi<br>ya pili katika<br>wingi wa<br>kiume | واو الجماعة-<br>الضمير<br>المخاطب الجمع<br>المذكر | mnaandika<br>(wengi, mm) |
| N <sub>2.wingi.kk</sub> | أنتنَّ | /taktabna/   | تُكْثِنَّ   | 'nuun ya kike'<br>kiambishi nafsi<br>ya pili katika<br>wingi wa kike         | نون النسوة-<br>الضمير المخاطب<br>الجمع المؤنث     | mnaandika<br>(wengi, kk) |

Kama tunavyoona hapo awali kuwa viambishi awali vinavyopatikana katika kitenzi cha wakati uliopo, huwa havibainishi nafsi ya mtenda, bali hubainisha hali ya wakati uliopo. Kwa mantiki hii, tunaweza kugundua kuwa kuna baadhi ya vitenzi vya wakati uliopo havina viambishi nafsi. Vitenzi hivyo ni vile ambavyo mtenda wake huwa katika nafsi ya kwanza katika umoja /?aktubu/ {أَكْتُبُ} ‘ninaandika’, nafsi ya kwanza katika wingi /naktubu/ {تَكْتُبُ} ‘tunaandika’, nafsi ya pili ya umoja wa kiume /taktubu/ {تَكْتُبُ} ‘unaandika’. Nafsi ya tatu katika hali ya umoja wa kiume /yaktubu/ {يَكْتُبُ} ‘aliandika’ pamoja na nafsi ya tatu ya umoja wa kike /taktubu/ {تَكْتُبُ} ‘aliandika’. Katika muktadha huu, hutumika kiambishi nafsi fiche ambacho huitwa kwa Kiarabu {ضَمِيرٌ مُسْتَترٌ}. Viambishi nafsi tamati vinavyoungana na vitenzi vya wakati uliopo ni hivi vifuatavyo:

a. Kiambishi nafsi tamati /ya/ kinachoitwa kwa Kiarabu /yaau muxa:t<sup>abat</sup>/ {يَا} ‘yau ya msemezwa’ inayoingizwa katika kitenzi cha wakati uliopo katika nafsi ya pili ya umoja wa kike /taktubi:na/ {تُكْثِنَّ} ‘unaandika’.

b. Kiambishi nafsi tamati /alifu/ kinachoitwa /?alif l-θnain/ {أَلْفُ الْاثْنَيْنِ} huingizwa katika kitenzi cha nafsi ya pili katika jinsia ya kiume /taktuba:ni/ {تُكْثِبَانَ} ‘wanaandika’, Pia, huingizwa katika kitenzi cha nafsi ya tatu katika hali ya uwili wa kiume /yaktuba:ni/ {يَكْثِبَانَ} na huingizwa katika kitenzi cha nafsi ya tatu katika hali ya uwili wa kike /taktuba:ni/ {تُكْثِبَانَ}.

c. Kiambishi nafsi tamati /nuun/ kinachoitwa /nuun l-nis-wat/ {نُونُ النُّسُوَةِ} ‘nuun ya kike’ hupachikwa katika kitenzi ambacho watenda wake ni wanawake wengi. Nuun ya kike hupachikwa katika nafsi ya pili ya wingi wa kike /taktabna/ {تُكْثِنَّ} na katika nafsi ya tatu ya wingi wa kike /yaktubna/ {يَكْثِنَّ}.

**Jedwali Na. 8 Kiambishi Nafsi katika Kitensi cha Wakati uliopo-Mtenda-N<sub>3</sub>**

| Kiwakilishi Nafsi | wakati uliopo | Kiambishi Nafsi | Tafsiri ya Kiswahili |
|-------------------|---------------|-----------------|----------------------|
|-------------------|---------------|-----------------|----------------------|

|                         |     |              |             |  |  |                            |
|-------------------------|-----|--------------|-------------|--|--|----------------------------|
| N <sub>3.umoja.mm</sub> | هو  | /yaktubu/    | يَكْتُبُ    | kiambishi nafsi<br>fiche cha nafsi ya<br>tatu katika umoja<br>wa kiume   | الضمير الغائب<br>المفرد المذكر،<br>مستتر<br>(هو) | anaandika<br>(mm)          |
| N <sub>3.umoja.kk</sub> | هي  | /taktubu/    | تَكْتُبُ    | kiambishi nafsi<br>fiche cha nafsi ya<br>tatu katika umoja<br>wa kike    | الضمير الغائب<br>المفرد المؤنث،<br>مستتر<br>(هي) | anaandika<br>(kk)          |
| N <sub>3.uwili.mm</sub> | هما | /yaktuba:ni/ | يَكْتُبانِ  | alifu ya uwili ni<br>kiambishi nafsi ya<br>tatu katika uwili<br>wa kiume | ألف الاثنين.-<br>الضمير الغائب<br>المثنى المذكر  | wanaandika<br>(wawili, mm) |
| N <sub>3.wingi.mm</sub> | هم  | /yaktubu:na/ | يَكْتُبُونِ | 'waau ya wingi'<br>kiambishi nafsi ya<br>tatu katika wingi<br>wa kiume   | واو الجماعة.-<br>الضمير الغائب<br>الجمع المذكر   | wanaandika<br>(wengi, mm)  |
| N <sub>3.wingi.kk</sub> | هنّ | /yaktubna/   | يَكْتُبُنِ  | 'nuun ya kike'<br>kiambishi nafsi ya<br>tatu katika wingi<br>wa kike     | ئون النسوة.-<br>الضمير الغائب<br>الجمع المؤنث    | wanaandika<br>(wengi, kk)  |

- a. Kiambishi nafsi tamati /alif/ kinachoitwa /Alif l-θnain/ {ألف الاثنين} ‘alifu ya uwili’ huingizwa katika kitenzi cha nafsi ya tatu katika hali ya uwili wa kiume /yaktuba:ni/ {يكتبان}.

b. Kiambishi nafsi tamati /waau/ ambacho kinaitwa /waau l-ʒama:qat/ {واو الجماعة} ‘wau ya wingi’ kinapachikwa katika kitenzi cha wingi wa kiume katika nafsi ya tatu /yaktubu:na/ {يكتبون}. Tuzingatie kuwa kiambishi tamati nuun {ن} kinachopatikana mwishoni mwa kitenzi cha wakati uliopo katika neno /yaktubu:na/ {يكتبون} siyo kiambishi nafsi tamati, kiambishi hicho huhusishwa na kiunganishi kinachosaidia kitenzi kubainisha wakati.

c. Kiambishi nafsi tamati /nuun/ kinachoitwa /nuun l-nis-wat/ {نون النساء} ‘nuun ya kike hupachikwa mwishoni mwa kitenzi katika nafsi ya tatu ambao watenda wake ni wanawake wengi wa kike /yaktubna/ {يكتبن}

### 3.5 Kiambishi Nafsi Wakati uliopo-Mtendwa

Kiambishi nafsi ya mtendwa ni kiambishi ambacho kinawakilisha mtu aliyefanyiwa kitendo. Kiambishi hiki hupachikwa mwishoni mwa kitenzi na huzingatia hali ya idadi na jinsia. Kwa hivyo, katika Kiarabu unaposema ‘umenjona mimi’ unaweza kusema {عُنْدَهُ} (Iqaab, 2019).

**Jedwali Na.9 Kiambishi Nafsi tamati katika Wakati uliopo-Mtendwa N<sub>1</sub> na N<sub>2</sub>**

**HALIMA ALI HASSAN: UCHUNGUZI WA MFUATANO WA VIAMBISHI NAFSI KATIKA VITENZI VYA KISWAHILI NA Kiarabu Kwa Kuzingatia Isimu Pambanuzi**

| Kiwakilishi Nafsi        |           | wakati uliopo                | Kiambishi Nafsi | Tafsiri ya Kiswahili   |
|--------------------------|-----------|------------------------------|-----------------|--|
| N <sub>1.umaja</sub>     | أَنَا     | /yad <sup>6</sup> ribuni:/   | يَضْرُبُنِي     | /ni:/<br>kiambishi<br>nafsi ya<br>kwanza<br>katika umoja<br>wa mtendwa<br>ني-<br>الضمير المتكلم<br>المفرد- دالة على<br>المفعول به                  |
| N <sub>1.wingi.</sub>    | نَحْنُ    | /yad <sup>6</sup> ribuna:/   | يَضْرُبُنَا     | /na:/<br>kiambishi<br>nafsi ya<br>kwanza<br>katika wingi<br>wa mtendwa<br>نا-<br>الضمير المتكلم<br>الجمع- دالة على<br>المفعول به                   |
| N <sub>2.umaja. mm</sub> | أَنْتَ    | /yad <sup>6</sup> ribuka/    | يَضْرُبُكُ      | /ka/<br>kiambishi<br>nafsi ya pili<br>katika umoja<br>wa kiume wa<br>mtendwa<br>كـ-<br>الضمير المخاطب<br>المفرد المذكر-<br>دالة على<br>المفعول به  |
| N <sub>2.umaja. kk</sub> | أَنْتِي   | /yad <sup>6</sup> ribuki/    | يَضْرُبُكِي     | /ki/ kiambishi<br>nafsi ya pili<br>katika umoja<br>wa kike wa<br>mtendwa<br>كـ-<br>الضمير المخاطب<br>المفرد المؤنث-<br>دالة على<br>المفعول به      |
| N <sub>2.uwili.</sub>    | أَنْتَمَا | /yad <sup>6</sup> ribukuma:/ | يَضْرُبُكُمَا   | /kuma:/<br>kiambishi<br>nafsi ya pili<br>katika uwili<br>كما-<br>الضمير المخاطب<br>المثنى- دالة على<br>المفعول به                                  |
| N <sub>2.wingi. mm</sub> | أَنْتُمْ  | /yad <sup>6</sup> ribukum/   | يَضْرُبُكُمْ    | /kum/<br>kiambishi<br>nafsi ya pili<br>katika wingi<br>wa kiume wa<br>mtendwa<br>كم-<br>الضمير المخاطب<br>الجمع المذكر-<br>دالة على<br>المفعول به  |
| N <sub>2.wingi. kk</sub> | أَنْتَنَّ | /yad <sup>6</sup> ribukunna/ | يَضْرُبُكُنَّ   | /kunna/<br>kiambishi<br>nafsi ya pili<br>katika wingi<br>wa kike wa<br>mtendwa<br>كـ-<br>الضمير المخاطب<br>الجمع المؤنث-<br>دالة على<br>المفعول به |

Kiambishi nafsi tamati /ni:/ {ني} hupachikwa katika kitenzi cha wakati uliopo katika nafsi ya kwanza katika umoja ili kubainisha kauli ya mtendwa /yad<sup>6</sup>ribuni/. Kiambishi nafsi /na:/ {نا} يَضْرُبُنِي .

upachikwa katika nafsi ya kwanza ya wingi /yad<sup>r</sup>ibuna:/ {يَضْرِبُنَا}. Kiambishi nafsi /ka/ {كَ} upachikwa katika nafsi ya pili ya umoja wa kiume/yad<sup>r</sup>ika/ {يَضْرِبُكَ}. Kiambishi nafsi /ki/ {كِ} hupatikana katika kitenzi cha nafsi ya pili katika umoja wa kike /yad<sup>r</sup>ibuki/ {يَضْرِبُكِ}. Kiambishi nafsi /kuma:/ upachika katika nafsi ya pili katika uwili /yad<sup>r</sup>ibukuma:/ {يَضْرِبُكُما}. Aidha, Kiambishi nafsi /kum/ {كُمْ} upachikwa katika kitenzi kinachobainisha nafsi ya pili katika wingi wa kiume /yad<sup>r</sup>ibukum/ {يَضْرِبُكُمْ} na kiambishi nafsi /kunna/ {كُنْ} upachikwa katika kitenzi cha nafsi ya pili katika wingi wa kike /yad<sup>r</sup>ibukunna/ {يَضْرِبُكُنْ}.

#### Jedwali Na.10 Kiambishi Nafsi wakati uliopo-Mtendwa N<sub>3</sub>

| Kiwakilishi Nafsi        | Wakati uliopo | Kiambishi Nafsi                                 | Tafsiri ya Kiswahili   |
|--------------------------|---------------|---|--|
| N <sub>3.umaja.</sub> mm | هو            | /yad <sup>r</sup> ibu/ <b>يَضْرِبُهُ</b>        | /hu/ kiambishi nafsi ya tatu katika umoja wa kiume wa mtendwa <b>هُ الضمير الغائب المفرد المذكر، دالة على المفعول به</b> anampiga (mm)             |
| N <sub>3.umaja.</sub> kk | هي            | /yad <sup>r</sup> ibuha/ <b>يَضْرِبُهَا</b>     | 'ha' kiambishi nafsi ya tatu katika umoja wa kike wa mtendwa <b>هَا- الضمير الغائب المفرد المؤنث، دالة على المفعول به</b> anampiga (kk)            |
| N <sub>3.uwili.</sub> mm | هما           | /yad <sup>r</sup> ibuhuma:/ <b>يَضْرِبُهُما</b> | /huma:/ kiambishi nafsi ya tatu katika uwili wa mtendwa <b>هُما- الضمير الغائب المثنى، دالة على المفعول به</b> anawapiga (wawili)                  |
| N <sub>3.wingi.</sub> mm | هم            | /yad <sup>r</sup> ibuhum/ <b>يَضْرِبُهُمْ</b>   | /hum/ kiambishi nafsi ya tatu katika wingi wa kiume wa mtendwa <b>هُم- الضمير الغائب الجمع المذكر، دالة على المفعول به</b> anawapiga (wengi, mm)   |
| N <sub>3.kk</sub>        | هنّ           | /yad <sup>r</sup> ibuhunna/ <b>يَضْرِبُهُنّ</b> | /hunna/ kiambishi nafsi ya tatu katika wingi wa kike wa mtendwa <b>هُنّ- الضمير الغائب الجمع المؤنث، دالة على المفعول به</b> anawapiga (wengi, kk) |

Kiambishi nafsi tamati /hu/ {ه} upachikwa katika kitenzi cha wakati uliopo katika nafsi ya tatu ya umoja wa kiume ili kubainisha dhana ya mtendwa /yad<sup>r</sup>ibu/ {يَضْرِبُهُ}. Kiambishi nafsi /ha:/ {ها} upachikwa katika nafsi ya tatu ya umoja wa kike /yad<sup>r</sup>ibuha/ {يَضْرِبُهَا}. Kiambishi nafsi /huma:/ hupatikana katika kitenzi cha nafsi ya tatu ya uwili wa kiume au kike /yad<sup>r</sup>ibuhuma:/ {يَضْرِبُهُما}. Aidha, Kiambishi nafsi /hum/ {هم} upachikwa katika kitenzi chenyé kubainisha nafsi ya tatu ya

kiume /yadribuhum/ {يَضْرُبُهُمْ} na kiambishi nafsi /hunna/ {هُنَّ} hupachikwa katika kitenzi cha nafsi ya tatu katika wingi wa kike /yadribuhunna/ {يَضْرُبُهُنَّ}.

#### **4.0 Matokeo ya Uchunguzi**

Kiswahili na Kiarabu ni lugha ambishi bainishi zinazoruhusu vitenzi vyake kubeba viambishi mbali mbali vinavyobainisha maumbo tafauti. Mfuatano wa viambishi nafsi huweza kujitokeza katika Kiswahili na Kiarabu kwa mujibu wa muktadha uliotumika. Tunaona kuwa kuna kufanana katika kigezo cha aina ya viambishi nafsi. Lugha zote mbili, Kiswahili na Kiarabu kuna aina tatu za viambishi nafsi vinavyoungana na kitenzi. Aina hizo ni nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu. Kila aina moja ya nafsi huwa na viambishi maalumu vinavyoungana na kitenzi. Viambishi hivyo huzingatia sifa ya umoja na wingi katika lugha zote mbili. Pia, kitenzi huweza kubeba kiambishi nafsi ya mtenda na mtendwa katika Kiswahili na Kiarabu. Aidha, viambishi nafsi katika Kiswahili na Kiarabu huweza kuwa na dhima zaidi ya moja. Mathalan, katika Kiswahili kiambishi awali /tu/ katika neno {tunasoma} huwa na dhima ya kubainisha nafsi ya kwanza ya mtenda katika hali ya wingi. Kwa upande wa Kiarabu, neno /yadribā:ni/ {يَضْرِبَانِ} ‘wanapigana’, kiambishi tamati /-aa/ kina dhima ya kubainisha nafsi ya tatu ya mtenda katika hali ya uwili.

Licha ya mfanano, ipo tafauti kubwa katika mfuatano wa viambishi nafsi katika kitenzi cha Kiswahili na Kiarabu. Tafauti hizo zinajitokeza katika kigezo cha idadi, jinsia, nafasi ya kiambishi katika neno na kutobebwa kwa baadhi ya viambishi vya nafsi katika kitenzi cha Kiarabu. Katika kigezo cha idadi, Kiarabu kina mfuatano mpana wa viambishi nafsi katika kitenzi. Kila aina moja ya nafsi huwa inabeba kiambishi nafsi chake kwa kuzingatia hali ya wakati. Kwa mfano, wakati uliopita huwakilishwa na viambishi nafsi tamati /tu/ {ثُ} katika nafsi ya kwanza ya umoja. Kiambishi nafsi /na:/ {نَا} hupachikwa katika nafsi ya kwanza ya wingi, kiambishi nafsi /ta/ {تَ} hupachikwa katika nafsi ya pili ya umoja wa kiume. Aidha, kiambishi nafsi /ti/ {تِ} hupachikwa katika nafsi ya pili ya umoja wa kike, kiambishi nafsi /tuma:/ {ثُمَّا} hupachikwa katika nafsi ya pili, kiambishi nafsi /tum/ {ثُمَّ} hupachikwa katika nafsi ya pili ya wingi wa kiume na kiambishi nafsi /tunna/ {ثُنَّ} hupachikwa katika nafsi ya pili katika wingi wa kike. Aidha, katika nafsi ya tatu, huwakilishwa na viambishi tamati /alif iθnain/ {أَلْفُ الْاثْنَيْنِ} ‘alifu ya uwili’ inayopachikwa katika nafsi ya tatu katika hali ya uwili, kiambishi cha /wau l-ʒama:cat/ {وَأَوْ الْجَمَاعَةُ ‘wau ya wingi’ hupachikwa katika nafsi ya tatu katika hali ya wingi wa kiume na kiambishi nafsi cha /nu:n l-nis-wat/ {نُونُ النِّسْوَةُ ‘nuun ya kike’ hupachikwa katika nafsi ya tatu ya wingi wa kike.

Ama kuhusu Kiswahili, hupachikwa kiambishi nafsi awali {ni-} katika hali ya umoja na kiambishi nafsi awali {tu-} katika hali ya wingi. Pia, hupachikwa kiambishi nafsi {u-} katika nafsi ya pili ya umoja na kiambishi nafsi {m-} katika wingi. Aidha, hupachikwa kiambishi nafsi {a-} katika nafsi ya tatu ya umoja na kiambishi {wa-} katika nafsi ya tatu ya wingi. Kutokana na mifano hiyo, tunagundua kuwa mfuatano wa viambishi nafsi katika Kiarabu ni mpana mno ukilinganishwa na Kiswahili.

Halikadhalika, katika Kiarabu viambishi nafsi huzingatia jinsia ya kike na kiume. Hali hii inaweza kupatikana katika nafsi ya pili ya umoja wa kiume, hupachikwa kiambishi nafsi /-ta/ nafsi ya pili ya umoja wa kike, hupachikwa kiambishi (-ti), nafsi ya pili ya wingi wa kiume, hupachikwa kiambishi /tum/ na nafsi ya pili ya kike hupachikwa kiambishi /tunna/. Katika nafsi ya tatu hupachikwa kiambishi nafsi cha waau ya wingi ambacho hubainisha wingi wa kiume na kiambishi nafsi /-na/ hubainisha wingi wa jinsia ya kike. Kwa kawaida, Viambishi nafsi hupatikana mwishoni mwa kitenzi katika Kiarabu tafauti na viambishi nafsi vya Kiswahili ambavyo hupatikana mwanzoni mwa kitenzi.

Pia, katika Kiarabu, maumbo ya vitenzi vya nafsi ya kwanza ya umoja na wingi pamoja na nafsi ya tatu ya umoja na wingi huwa hayabebi viambishi nafsi. Aidha, viambishi nafsi katika Kiarabu hubadilika kwa kuzingatia hali ya wakati wa kitendo sifa ambayo haipatikani katika Kiswahili.

## 5.0 Hitimisho

Mfuatano wa viambishi nafsi katika Kiarabu umeshikamana na jinsia ya kiume na kike, idadi ya umoja, uwili na wingi pamoja na kuzingatia hali ya mtenda na mtendwa. Aidha, viambishi nafsi katika Kiarabu, huzingatia wakati wa kitendo uliopita na wakati uliopo na viambishi hivyo vinapatikana mwishoni mwa kitenzi. Katika Kiswahili, viambishi nafsi huzingatia hali ya idadi ya umoja na wingi pamoja na kuzingatia hali ya mtenda au mtendwa. Kutokana na ubainifu huu, tunaona kuwa mfuatano wa viambishi nafsi katika Kiarabu ni mpana mno ukilinganisha na Kiswahili. Hali hii inathibitisha kuwa Kiswahili na Kiarabu zinafanana katika baadhi ya miundo na zinatafuatiana katika miundo mengine. Kila lugha ina mfumo wake wa upachikaji wa viambishi. Kwa mantiki hii, tafiti zaidi zinaweza kufanyika ili kubaini michakato ya upachikaji wa viambishi ili kugundua kiwango cha kufanana na kutafautiana.

## Marejeleo

- Attia, M. A. (2002). Implication of the Agreement Feature in Machine Translation: M. A. in Faculty of Languages and Translation, Al-azhar University, Cairo-Egypt: imepatikana katika <https://www.academia.edu>.
- Bosha, I. A. (1993). Taathira za Kiarabu katika Kiswahili pamoja na Kamusi Thulaathiya, Kiswahili, Kiarabu na Kiingereza: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Chomsky, N. (1957). Aspects of the Theory of Syntax. Cambridge, Mass MIT Press.
- Firmansyah, N. I. (2022). A Contrastive Study of English and Arabic Verb Morphology. imepatikana katika <http://digilib.uinkhas.ac.id>.
- Hakimu, J. (2020). Ubantuishaji wa Kimofolojia katika Vitenzi vya Kiswahili vyenye Asili ya Kiarabu. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu: Chuo kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Hahn, M. (2011). Null Conjunctions and Bound Pronouns in Arabic. Proceedings of the 18<sup>th</sup> International Conference on Head-Driven Phrase Structure Grammar (pp. 60-80). University of Washington: CSLI Publication.
- Iqaab, Z. K. (2019). Pronoun in English and Arabic: A Contrastive Study. English Language and Literature Studies (pp. 53-69). Iraq: Canadian Center of Science and Education.
- Japensarage, M. A. & Kasiyarno, M. H. (2015). Arabic Personal Pronouns as Word, Clitic, and Affix. International Journal on Studies in English Language and Literature (IJSELL) Volume 3, Issue 2, pp 33-41. imepatikana katika [www.arcjournals.org](http://www.arcjournals.org).
- Kihore, Y. M. & Massamba, D. P. B. & Msanjila, Y. P. (2001). Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA). Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).
- Krumm, B. (1940). Words of Oriental Origin in Swahil. The Sheldon Press.
- Lodhi, A.Y. (2000). Oriental Loans in Swahil Study in Language and Culture Contacts. Gothenburg.
- Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M. & Hokororo, J. I. (2012). Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Massamba, D. P. B. (2016). Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugh. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.
- Massamba, D. P. B. (2017). Historia ya Kiswahili: Mtazamo Mpya 100KK hadi 2000 B.K. Dar es Salaam: Kiswahili Development Limited.

| Arabic Script     | IPA symbol | Symbols used in IVAr |
|-------------------|------------|----------------------|
| <b>Consonants</b> |            |                      |
| أ - الهمزة        | ?          | 2                    |
| ب                 | b          | b                    |
| ت                 | t          | t                    |
| ث                 | θ          | th                   |
| ج                 | ʒ          | j                    |
| ح                 | ħ          | H                    |
| خ                 | x          | x                    |
| د                 | d          | d                    |
| ذ                 | ð          | dh                   |
| ر                 | r          | r                    |
| ز                 | z          | z                    |
| س                 | s          | s                    |
| ش                 | ʃ          | sh                   |
| چ                 | tʃ         | ch                   |
| ص                 | s'         | S                    |
| ط                 | t'         | T                    |
| ض                 | d'         | D                    |
| ظ                 | ð', z'     | DH, Z                |
| ع                 | ʕ          | 3                    |
| غ                 | ɣ          | gh                   |
| ف                 | f          | f                    |
| ق                 | q          | q                    |
| ك                 | k          | k                    |
| گ                 | g          | g                    |
| ل                 | l          | l                    |
| م                 | m          | m                    |
| ن                 | n          | n                    |
| ه                 | h          | h                    |
| و                 | w          | w                    |
| ي                 | j          | y                    |
| و                 | v          | v                    |

| Vowels |        |        |
|--------|--------|--------|
| ا      | a:     | a:     |
| ي      | i:, e: | i:, e: |
| و      | u:, o: | u:, o: |
| فتحة   | a      | a      |
| كسرة   | i      | i      |
| ضمة    | u      | u      |

Other symbols:

|                                    |   |
|------------------------------------|---|
| gemination                         | double the letter (e.g. 2alla:h)  |
| al-                                | assimilate the l- when it is assimilated<br>e.g. lwalad TTawi:l   |
| attach<br>prepositions to<br>nouns | Examples:<br>minil madi:na (من المدينة)<br>fil be:t (في البيت)<br>b3ishri: (عشرين)<br>fiTTari:g (في الطريق) |